



Taarifa kwa Vyombo vya Habari

5 Julai 2016

Nusu ya wananchi wa Tanzania Bara hawafahamu kilichojiri Zanzibar tangu uchaguzi mkuu Wananchi 4 kati ya 10 wanasema Rais aliyechaguliwa kwenye uchaguzi mpya akubalike kuwa Rais halali

5 Julai 2016, Dar es Salaam: Zanzibar ilikumbwa na matukio mengi wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 2015. Matokeo ya uchaguzi yalifutwa baada ya mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kusema "kulikuwa na ukiukwaji wa sheria ya uchaguzi." Uchaguzi mpya ulipangwa kufanyika mwezi Machi 2016. Maamuzi hayo yalipingwa vikali na upinzani na kutiliwa shaka na mionganini mwa wajumbe wa jumuia ya kimataifa. Viongozi wa upinzani pamoja na wafuasi wao waligoma kushiriki kwenye uchaguzi mpya. Matokeo yake mgombea wa Chama Cha Mapinduzi aliyekuwa madarakani Rais Ali Mohamed Shein akaibuka na ushindi kiurahisi.

Pamoja na matukio hayo, nusu ya wananchi wa Tanzania Bara (53%) wanasema hawafahamu kile kilichojiri Zanzibar tangu ulipofanyika uchaguzi mkuu wa Oktoba. Wananchi 4 kati ya 10 wana taarifa kuwa uchaguzi mpya ulifanyika tarehe 20 Machi 2016 (43%) na wanafahamu kuwa matokeo ya uchaguzi mkuu wa Oktoba yalifutwa (39%).

Matokeo haya yametolewa na Twaweza kuitia muhtasari wa utafiti wake wenye kichwa cha habari, "Masuala ya Muungano: Maoni ya wananchi kuhusu kinachoendelea Zanzibar". Muhtasari huo unatokana na takwimu zilizokusanywa na *Sauti za Wananchi*, Utafiti wa kwanza barani Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa na unaotumia simu za mkononi. Matokeo haya yanatokana na takwimu zilizokusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,815 kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara (Zanzibar haihusiki kwenye matokeo haya) kati ya tarehe 29 Machi na tarehe 12 Aprili 2016.

Wananchi wa Tanzania Bara wametoa maoni yao kuhusu nini kifanyike kutatua mgogoro uliopo. Takribani nusu ya wananchi (42%) wanasema Rais aliyechaguliwa kwenye uchaguzi mpya wa tarehe 20 Machi 2016 atambulike kuwa Rais halali. Na ni 20% pekee ya wananchi wanasema uchaguzi mpya wa tarehe 20 Machi ulikuwa ni hatua nzuri ya kutatua mgogoro.

Baadhi ya mapendekezo ya wananchi ni pamoja na kumtangaza mgombea urais wa chama cha CUF - Seif Shariff Hamad - kuwa mshindi wa uchaguzi wa Oktoba 2015 (14%), kuunda serikali ya umoja wa kitaifa (13%) na kufanya mazungumzo kutafuta ufumbuzi wa amani (8%).

Mkurugenzi mtendaji wa Twaweza Aidan Eyakuze, anasema "*Serikali ya Muungano, na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zina kazi kubwa ya kurejesha umoja baina ya wapiga kura visiwani Zanzibar. Lakini inatia wasiwasi kubaini kwamba idadi kubwa ya watanzania walikiri kutojua kilichotokea Zanzibar baada ya uchaguzi wa Oktoba 2015. Hali hii inaudhoofisha Muungano wetu. Tukitaka kuudumisha, hatuna budi kama wananchi, kuufuatilia kwa karibu sana.*"

---- Mwisho ----

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:

Risha Chande

Mshauri Mwandamizi wa Mawasiliano, Twaweza

e: rchande@twaweza.org | Simu: (+255) (0) 656 657 559

Maelezo kwa Wahariri

- Muhtasari huu na takwimu zake zinapatikana kupitia www.twaweza.org, au www.twaweza.org/sauti
- Twaweza inafanya kazi ya kupima uwezo wa watoto kujifunza, wananchi kuwa na utayari wa kuleta mabadiliko na serikali kuwa wazi zaidi na sikuvi katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Twaweza ina programu, wafanyakazi na ofisi katika nchi zote tatu, na utaratibu unaoheshimika kimataifa wa kujifunza, ufuatiliaji na tathmini. Programu zetu muhimu ni pamoja na Uwezo, tathmini kubwa ya kila mwaka ya wananchi barani Afrika inayopima viwango vya watoto vya kujifunza kwenye maelfu ya kaya, na Sauti za Wananchi, utafiti wa kwanza Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika kwa njia ya simu ya mkononi. Pia tunashiriki kwenye masuala ya umma na sera, kupitia ubia wetu na vyombo vya habari, juhudhi za kimataifa zinazoshughulikia masuala ya uongozi kama vile mpango wa Ushirikiano na Serikali wazi (OGP).

Tovuti: www.twaweza.org **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twita:** @Twaweza_NiSisi